

## Maswali na Majibu

1. Tukisema uongo, nani huwa anajua chenye tumefanya? *Mungu*
2. Anania na Safira walipanga kufanya nini?  
*Kuuza shamba lao. Wapee maskini sehemu ya hizo pesa na kuweka zingine. Lakini walijifanya kwamba wamepeana hizo pesa zote.*
3. Kulikuwa na kosa kwa wao kujiwekea sehemu ya pesa?  
*Hapana. Pesa zilikuwa zao na wangepanyia walichotaka.*
4. Walifanya nini iliyoonekana ni makosa?  
*Walidanganya Mungu na kwa wandugu na wadada.*
5. Nini ilifanyika kwa Anania na Safira? *Walianguka chini na wakafa.*
6. Ni vizuri kuchukua vitu vidogo vya wenzetu?  
*Hapana. Ni makosa kuiba vitu vya wenzetu hata kama ni vidogo au vikubwa.*
7. Hongo ni nini?  
*Kulipa mtu akufanyie kitu kimakosa. Ama kuchukua pesa kutoka kwa mtu ili umfanyie kitu cha makosa.*
8. Peana mifano 3 vile tunaweza kuwa waaminifu katika maisha yetu.  
*Sema ukweli wakati wote. Usichukue hongo wala upeane. Usidanganye wala kuiba.*
9. Nini itafanyika ikiwa tutahubiri uaminifu na huku sisi wenyewe si waaminifu?  
*Watu hawataamini yale tunayohubiri. Tutaleta aibu kwa Jina la Mungu.*
10. Watu wa aina gani watakuwa kwa Ufalme?  
*Angalia maneno yaliyofungwa pale juu ya somo la Zaburi 15.*

## Mistari ya kukariri

Zaburi 101:7      Zaburi 139:1 – 4      Zaburi 15:1 – 2

## Mazungumzo

Zungumza au igiza mchezo wa vile unaweza kudanganya, kuiba, kusema uongo au chukua hongo. Unaweza kushinda haya majaribu namna gani na uwe tofauti?

## Kuandika

Andika hadithi ya Anania na Safira. Hii hadithi inatufunza nini?

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



## Somo la 47 Uaminifu

**SOMA** Mithali 12:22; Zaburi 101:7; Zaburi 139:1 – 4; Matendo 5:1 – 11;  
Zaburi 15:1 – 5; Mithali 11:1

### SOMO

Mungu ni Mungu wa ukweli. Njia Zake zote ni za kweli. Mungu ni kama mwamba; Yeye ni wakutegemewa kabisa na kweli kwa kila kitu afanyalo na asemalo. Tunategemea ahadi za Mungu kwamba ni za ukweli. Tunaamini kwamba hatasema uongo wala kutudanganya.

Uaminifu ni sehemu ya maana sana kwa maisha ya Mkristo. Hatuwezi kuishi na kuabudu pamoja kama hatuaminiani. Biblia inatwambia vile ni muhimu sana kuwa waaminifu kwa kila jambo katika maisha yetu. Mungu hapendi kudanganya na kutoaminika.

Tunadanganya kwa sababu tunafikiri kwamba tutaheba. Tunafikiri kwamba hakuna atakayejua ukweli. **Wakati wote** Mungu anajua lile tufanyalo na kusema hata na kuwaza. Hatuwezi kuficha lolote kutoka kwa Mungu.

Anania na mkewe Safira walikuwa Wakristo katika kanisa ya kwanza. Walifikiri watadanganya wandugu na wadada hata na Mungu. Wakati huo, Wakristo wengi waliuza mashamba na nyumba ili wasaidie maskini.

Anania na Safira walitaka Wakristo wenzao wafikirie kwamba wao ni wazuri sana. Walikuwa ni watu waliozungumzia mazuri waliyoyafanya. Wangepaidia mtu wakati watu wamewaona yaani hadharani. Yesu alisema tusijaribu kufanya watu waone kwamba sisi ni wazuri. Tufanye mambo mazuri kuonyesha upendo kwa Mungu.

Anania na Safira waliona Wakristo wengi waliuza nyumba na mashamba zao wakipeleka pesa ili iwasaidie maskini. Walifikiri kwamba watu watawaona wao ni wazuri sana wakiuza shamba lao ili wasaidie maskini. Walitaka watu wawaone ni wazuri sana – lakini hawakutaka kupeleka pesa zote. Walifanya mpango wa kudanganya wandugu na wadada. Walidhani hakuna atakaejua uongo wao. Walisahahu kwamba mtu hatafanya lolote na Mungu asijue.

Anania na Safira waliuza shamba lao kwa pesa nyingi sana. Mpango wao ulikuwa wapeleke pesa zingine kusaidia maskini na wajiwekee zingine. Haikuwa kosa wao kufanya hivyo. Mpango wao ulikuwa mbaya kwa sababu walidanganya juu ya pesa walizopata. Walisema kwamba wamesaidia maskini pesa **zote** walizopata lakini walificha zingine.

Anania alipelekea Petro sehemu kidogo ya pesa. Aliambia Petro, “Tumeuza sehemu ya shamba. Tumeleta pesa **zote** ili zisaidie maskini.” Anania alifikiri kwamba Petro, wandugu na wadada wataona kwamba wao ni wazuri.

Anania alisahahu kwamba Mungu anajua kila kitu tufanyayo na kila kitu tufikiriayo. Tunaweza kudanganya wandugu na wadada lakini hatuwezi kudanganya Mungu. Mungu alijua mpango wenye Anania na Safira walikuwa nao. Alijua kwamba Anania alikuwa anadanganya. Mungu alionyesha Petro mpango wenye Anania alikuwa amefanya.


Petro alikasirika sana. Aliambia Anania, “Mbona umemdanganya Mungu? Shamba lilikuwa lako. Ukaamua kuuza. Mungu angefurahi kwa kuwapa maskini pesa. Hakukuwa na makosa kujiwekea sehemu ya pesa. Lakini ulitaka kudanganya watu na kujionyesha kwamba wewe ni mzuri. Umedanganya Mungu.” Papo hapo Anania alianguka china na kukufa. Kulikuwa na vijana waliokuja wakamfunga. Walimchukuwa na kwenda kumzika.

Baada ya masaa tatu Safira alikuja kwa Petro. Hakujua kilicho mtokea Anania. Petro alimuuliza, “Hii ndiyo pesa mlipata baada ya kuuza shamba?” Safira alidanganya Petro kwa kusema hizo ndizo pesa zote wameleta zisaidie maskini. Petro alimwambia, “ Mbona nyote mmepanga kumdanganya Mungu?” Safira naye alianguka chini na kufa. Alizikwa kando ya mme wake.

Ni rahisi sana kujifanya tuonekane wazuri, lakini kweli mioyoni tuko tunadanganya. Tusijifanye tunapea Mungu kila kitu na kujiwekea sisi wenyewe sehemu. Haikukuwa makosa Anania na Safira kujiwekea sehemu nyingine ya pesa. Kama wangekuwa waaminifu kwa walichofanya. Mungu angekubali. Makosa waliyofanya ni kudanganya Petro na Mungu.

Tukitenda dhambi tunaweza kuwa tunaumiza wenzetu, lakini cha muhimu zaidi ujue kwamba unatenda dhambi mbele ya Mungu. Wakati huu Mungu hauwi papo hapo vile aliwa Anania na Safira. Lakini Yesu atakapokuja kusimamisha Ufalme wa Mungu, watu wasiowaaminifu wataadhibiwa.

Biblia inatufundisha kuwa waaminifu kwa vitu vikubwa na vitu vidogo. Lazima tuwe waaminifu kwa hali na njia zote. Mithali 11:1 inatwambia kwamba Mungu hapendi mizani isiyo ya kweli. Anapenda mizani iliyo sawa kwa kupimia uzito.



Fikiria, mwenye duka anayebadilisha mizani yake kusudi ili apimie mteja uzito wa chini ukilinganisha na anayolipa. Mwenye duka anafikiria kwamba yeye ni mwerefu, lakini ajue Mungu hapendi usiwe mwaminifu.

Hata na sisi tunaweza kuwa tunadanganya watu kwa njia zingine. Tunaweza kudanganya kwamba sisi ni wagonjwa ili tusiende kusaidia wenzetu. Tunaweza kudanganya ili tusipatikane kwa makosa. Tunaweza kujifanya mbele ya watu kwamba sisi ni wazuri kwa mtu fulani lakini ukweli sisi ni wabaya sana kama watu hawako. Tunaweza kuiba vitu kwa shule au mahali tunafanya kazi – kama kalamu au karatasi. Kuchukua kitu chochote chenye si chako ni kuiba, hata kama ni kidogo au kikubwa.

Hongo ndiyo mbaya sana kwa uaminifu. Hongo ni kulipa mtu afanye makosa au asiwe mwaminifu. Au mtu anaweza kutupea pesa ili tufanye kitu kisichotakiwa. Ni makosa kuchukua au kupeana hongo. Mungu hapendi hongo na anasema wote wanaofanya hivyo hawataingia kwa Ufalme Wake.

Kuna sababu ingine yakufanya Wakristo wawe waaminifu kabisa. Watu wataangalia kwa umakini ili waone kama tunafanya tunayohubiri au la. Tukiwa waaminifu, watu wataona kumbe kweli tunafanya tunayohubiri. Tukihubiri uaminifu na hali hatuaminiki kwa maisha yetu, watu hawataamini maneno ya Mungu tunayohubiri. Tutaleta aibu kwa Jina la Mungu.

*Katika Zaburi 15, Mungu anatwambia ni watu waaina gani wanatakiwa wawe kwa Ufalme Wake:*

- ◆ Wanafanya haki kwa kuweka amri za Mungu.
- ◆ Wanazungumza ukweli kila mara. Wanasema chenye kweli wanafikiria.
- ◆ Hawazungumzi mambo mabaya juu ya wenzao.
- ◆ Wanaheshimu wale wanaopenda Mungu na kumwabudu.
- ◆ Hawashiriki na wale wanaokataa amri za Mungu.
- ◆ Wanazingatia maneno yao bila kuvunja ahadi zao hata kama inaumiza.
- ◆ Hawadanganyi wengine.
- ◆ Hawatumii hongo.

Kawaida Mungu hutimiza haki yake kwa uaminifu kwa wale watu wanaoweka ahadi zake. Hatuwezi kutarajia Mungu atukubali kwa Ufalme Wake kama si waaminifu na tunadanganya watu. Tuombe Mungu atusaidie tuwe waaminifu kwa hali zote katika maisha yetu.